

# MRENO KAFUKUZWA KATIKA MKUTANO

Geneva — Switzerland, Alhamisi.

**M**JUMBE WA URENO KATIKA MKUTANO WA ELIMU WA MATAIFA YOTE ALITOLEWA BAADA YA WAJUMBE KUTOKA AFRIKA KUPINGA KUWAKO KATIKA MKUTANO HUO KWA SABABU YA SIASA YAO YA UBAGUZI INAYOENDESHWA KATIKA NCHI ZA AFRIKA, ANGOLA NA MSUMBIJI.

Kura 40 kwa, 23 ziliamua kufukuzwa kwake baada ya azimio la Waafrika kwamba Ureno inawaweka wanchi wa huko katika hali ya ujinga kwa kuwanyima haki zao za ubinadamu.

Wajumbe wote wa Kia-rabu, Uyahudi, Afrika na Kirusi walipiga kura kumtoa Mreno na nchi nyingi za Ulaya, Japan, na Amerika ya Kusini zikipinga azimio hilo.

## Watimka

Wiki iliyopita Wajumbe wa Kiafrika na Kiaarabu walisusa mkutano wa mambo ya kazi (ILO) wakipinga kuwepo kwa mjumbe wa Afrika ya Kusini. Kwasababu katiba ya chama hicho hairuhusu wajumbe kumtoa mjumbe mwenzao, ilikuwa vigumu kwa Kaburu kufukuzwa, lakini hata hivyo Kaburu alikatazwa katika mambo mengine yote.

Mjumbe huyo wa Ureno baada ya kufukuzwa aliwambia waandishi wa habari kwamba nchi yake itakata rufaa kwenye Baraza Kuu la sheria Ulimwengu ni.

Azimio hilo la Afrika kuitaka Ureno ifukuzwe lilitolewa na Waziri wa Elimu katika nchi ya Nigeria,

Bw. Aja Nwachuku siku ya Jumatatu mkutano ulipofunguliwa.

Azimio hilo limesema wazi kwamba kuwepo kwa Mreno katika mkutano huo ni kosa kwa haki za binadamu na watoto, na pia ni kinyume cha haki za elimu.